

Ah Peter!
Ni kosa
gani hili!

Rafiki
gani wewe!

Na hajui kuwa
nilishindwa mtihani
wangu wa hesabu!

Hata
mbwa
ananichukia!

Mungu
anakupenda!

Hapana!
Mungu angeweza
kunipenda?

Mungu
anakupenda!

Kweli?

Peter akageuza ukurasa, na hichi ndicho alisoma.

MUNGU ANAKUPENDA!

Warumi 5:8
 Yohana 3:16
 1 Yohana 4:16



MUNGU ALIKUUMBA!

Analijua jina lako, ulizaliwa lini, unapoishi, kila kitu kuhusu wewe.

Mungu ana upendo maalum kwa ajili yako!



Warumi 3:23

Dhambi yetu hututenganisha na Mungu.

uango
 mtazamo mbaya
 mapigano

kudanganya
 kuwa mbinafsi

Sisi sote tumetenda dhambi. Ni Mungu tu anayeweza kutusamehe na kutufanya kuwa sehemu ya familia yake. Kwa msaada wake, tunaweza kusema "HAPANA!" kutenda dhambi.



Yesu Kristo, Mwana wa Mungu, alikufa kwa ajili yako.

Warumi 6:23
 Yohana 14:6



Kisha akafufuka, akaja hai tena.

Mungu alimtuma Yesu, Mwanawe, kulipa bei ya dhambi zako. Unapomwamini Yesu na kukiri dhambi zako, anakusamehe na anakupa maisha mpya kwa sababu sasa wewe ni mmoja wa familia yake. Yohana 1:12

Ili kumpokea YESU kama Mwokozi wako, fanya mambo haya matatu:

1. Mwambie Mungu kwamba kwa moyo wako wote unaamini kuwa Yesu Kristo ni Mwana wake. Mwambie unaamini Yesu alikufa mahali pako na akaja hai tena.

Warumi 10:9-10

2. Kiri kwamba umefanya dhambi na umemwasi. Mwombe Mungu akusamehe dhambi zako. 1 Yohana 1:9

Waefeso 2:8-9

3. Mwulize Yesu aje maishani mwako kama Mwokozi wako na Mfalme. Mwulize akusaidie kutii Biblia na kuishi kwa ajili yake maisha yako yote.

Wakolosai 2:6

Mpende Mungu kwa moyo wako wote.



Mungu ananipenda! Ninaamini Yesu ndiye Mwana wa Mungu. Nataka kumpa maisha yangu.

Acha tuzungumze na Mungu.

Mama, Mungu ananipenda. Amenisamehe. Kwa msaada wake, naweza kuwa mtiifu na mwenye furaha.

Unaweza kupokea upendo wa Mungu na msamaha katika Yesu, Mwana wa Mungu. Mwamini Yesu Kristo sasa hivi.

Jifunze zaidi juu ya Mungu
Soma Biblia yako • Ongea na Mungu kila siku



Ili kumwomba Yesu kuwa Mwokozi wako, unaweza kuongea na Mungu ukitumia maneno yaliyoandikwa hapa. Sema sala hii kutoka moyoni mwako. Mungu atakusikia na kukujibu.

Mungu Mpendwa, Muumba wangu,

Asante kwa kunipenda. Ninaamini moyoni mwangu kuwa Yesu Kristo ni Mwana wako. Ninaamini alichukua adhabu ya dhambi zangu wakati alikufa msalabani na akaja hai tena.

Ninagundua nimetenda dhambi na nimefanya mambo yasiyofaa. Sijatii. Tafadhali unisamehe na vondoe hatia yangu na aibu. Nipe nguvu ya kusema "Ndiyo" kwako na "Hapana" kwa vitu vibaya.

Bwana Yesu, tafadhali njoo maishani mwangu kama Mwokozi wangu na Mfalme. Nataka kukutii. Unisaidie kukufuata na kujifunze zaidi juu yako ninaposoma Biblia kila siku. Unifundishe jinsi ya kuishi kwako. Unifanye niwe sehemu ya familia yako. Wewe ni Mungu wangu, na mimi nakuabudu. Ninakupenda!

Saini, Mtoto Wako _____

(Andika jina lako)

Tarehe _____